MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA
KAS MASH MAGH KUS
JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 18. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Machi 21-31, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 1-10, 2019**

**Muhtasari**


- Mvua za msimu zinazoendelea zitasaidia kuongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao
- Mvua za msimu wa masika kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zinatarajiwa kupungua katika wiki ya pili ya mwezi April hivyo wakulima na wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki.
- Wakulima, Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kwenye shughuli zao.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hii ilisababisha msukumo wa ukanda wa mvua Inter-Tropical Convergence Zone (ITCZ) kutoka kusini na kufika katika maeneo ya kusini mwa Tanzania. Joto la bahari la juu ya wastani liliendelea katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la chini ya wastani lilipimwa katika eneo la Rasi ya Msumbiji hivyo kusababisha makutano ya upepo kusini mwa nchi. Katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kuchangia katika kufanyika kwa vimbunga baharini. Joto la bahari la juu wastani lilikuwa katika eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ilisababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Katika kipindi hiki cha siku kumi (dekadi), maeneo mengi ya nchi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yalipata mvua za kiasi cha milimita 26 hadi 150 isipokuwa eneo la kusini mwa mkoa wa Lindi ambalo lilipata milimita 200. Hata hivyo baadhi ya maeneo ya mikoa ya Dodoma na Singida yalipata mvua chini ya milimita 26. Kwa upande wa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka maeneo mengi yalipata mvua kati ya milimita 26 hadi 100 isipokua baadhi ya maeneo ya mkoa wa Manyara na Arusha ambapo yalipata mvua chini ya milimita 26 kama inavyoonekana katika ramani.




Kielelezo:1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 21- 31, 2019.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Katika kipindi hiki cha dekadi, maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa. Hata hivyo, katika mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora maendeleo ya ukuaji wa mahindi umeathiriwa kutokana na vipindi virefu vya ukavu vilivyojitokeza katika maeneo hayo.

Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka vipindi vya ukavu vilionekana ndani ya kipindi cha nusu ya kwanza ya dekadi hususan katika mikoa ya Kilimanjaro, Moshi, Same, Kiteto, Pwani na visiwa vya Unguja na Pemba ambapo hali hiyo iliathiri ukuaji wa mazao. Hata hivyo katika mkoa wa Kagera hususan wilaya ya Bukoba maeneo mengi yaliendelea kupata mvua ambazo zilisaidia ukuaji wa mazao. Hali ya maji na malisho ya wanyama yalikua katika hali nzuri kwa ujumla katika maeneo mengi ya nchi.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka kidogo kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberian) inatarajiwa kuimarika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo maeneo ya kusini mwa nchi yetu. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayopelekea kuwepo kwa kimbunga ambacho kitasababisha ongezeko la mvua maeneo ya magharibi mwa nchi na maeneo yote ya kusini mwa nchi na kupunguza uwezekano wa mvua maeneo ya pwani ya Kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii haitarajiwi kusababisha mabadiliko makubwa ya mifumo ya hali ya hewa katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019

Kanda ya ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na nyanda za juu Kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo zinatarajiwa kuendelea. Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) vipindi vya mvua vinavyoambatana na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache. Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) mvua zinazoambatana na ngurumo zinatarajiwa katika maeneo machache hususan nusu ya kwanza ya dekad.Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo zinatarajiwa hususan nusu ya kwanza ya dekad. Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache zinatarajiwa kuendelea.

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 01-10,2019

Mvua za msimu zinazoendelea zitasaidia kuongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao ya muda mfupi na yanayohitaji mvua kidogo. Hata hivyo, mvua za msimu wa masika kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zinatarajiwa kupungua katika wiki ya pili ya mwezi Aprili hivyo wakulima na wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki. Wakulima, Wafugaji na wavuvi wanashauriwa pia kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kwenye shughuli zao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 01-10, 2019.

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***